

Usemezano Katika Kilio Cha Haki

Joseph Murithi Jessee

(Kenya University)

Corresponding Author: Joseph Murithi Jessee

Date of Submission: 24-09-2018

Date of acceptance: 13-10-2018

UTANGULIZI

Katika makala hiitumejadili usemezano katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki*(Mazrui, 1981). Hii ni kutokana na kauli ya Bakhtin (1981) kwamba usemezano haupatikani katika tamthilia bali hupatikana katika riwaya. Tunalenga kuangazia ni kwa namna gani usemezano umewasilishwa katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki*. Tutaangazia vile ambavyo Mazrui ametumia Sajili mbalimbali, mivutano baina ya “mimi” na “yeye”, lugha ya wahusika, utumizi wa matini zingine na masimulizi ya urejeleaji ya moja kwa moja ya kifasihi katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Sifa hizi ndizo Bakhtin(1981) anasema kwamba hazipatikani katika tamthilia na kwa hivyo hakuna usemezano katika tamthilia.

MUHTASARI WA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI

Tamthilia ya *Kilio Cha Haki* inashughulikia udhalimu wa makaburu, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, utetezi wa haki za wafanyikazi na ukombozi wa akina mama. Huku akifuata mtazamo wa uyakinifu wa kijamaa Mazrui anawasiri jamii ya Kiafrika kama jamii ambayo inakumbwa na matatizo chungu nzima.

Mhusika wake mkuu Lanina ni mwanamke anayekandamizwa maradufu kama mwanamke na mfanyikazi. Amemchora kama mtetezi wa wafanyikazi na mtetezi dhidi ya dhuluma kwa wanawake. Lanina anaongoza mgomo kwanza katika shamba la Rhodeman na pili katika shamba la Delamon na kufanikisha mapinduzi ambapo Delamon, Tereki, Pelekha na Matovu wanauawa. Lanina anawekwa kizuizini lakini watu wamepata moyo na ari ya kupigania ukombozi wao na wataendelea kufanya hivyo. Lanina anafaulu kuwazindua wafanyakazi wenzake wapambane na udhalimu na watetezi haki zao.

Mazrui ameonyesha mapambano baina ya wafanyikazi na udhalimu wa makaburu waliovamia nchi yao. Aidha ukoloni na ukoloni mamboleo yameonyeshwa kama matatizo yanayozikumba nchi za Kiafrika. Ukombozi wa kina mama pia umesisitizwa sana katika tamthilia hii. Mazrui (1981) amefanya hivyo kwa kuzingatia historia ya jamii, uhalisi wa matukio na wahusika na mtazamo wa kimapinduzi ambao unasababishwa na ukinzani wa matabaka na mfumo wa ushalishaji maji. Amewasilisha ukweli kama unavyoweza kupatikana katika jamii za Kiafrika na za kiulimwengu.

SAJILI MBALIMBALI

Katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki*, kuna matumizi ya sajili tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe. Baadhi ya sajili hizi ni sajili ya magazeti, sajili ya sheria, sajili ya mashairi na nyimbo, sajili ya mazungumzo na kadhalika. Bakhtin (1981) anasema kwamba ni katika matumizi ya sajili tofauti ambapo usemezano huweza kupatikana katika matini

Mazrui ametumia sajili ya magazeti katika kutueleza habari kuhusu Lanina katika sehemu ya kwanza. Amewasawiri Dewe na Musa wakisoma gazeti. Kwanza habari muhimu kuhusu kushikwa kwa Lanina zimeandikwa mwanzo. Habari hizi ni muhimu kwani huyu ni mwanamke aliyeongoza mgomo mkubwa uliosababisha kuawa kwa akina Delamon, Tereki, Pelekha na Matovu, yaani makaburu na wasaliti wa wafanyikazi. Pia ni habari muhimu kwa watu kama Dewe na Musa ambao walikuwa wametoroka baada ya mgomo huu. Aidha, kichwa chake kimeandikwa kwa herufi kubwa “LANINA KUPELEKWA MAHAKAMANI” (uk. 2) na kwa mkato. Lugha iliyotumika ni sawa kisarufi na sentensi zake ziko katika taarifa. Kwa hivyo, mwandishi ametumia sajili ya magazeti katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981) kuendeleza ujumbe na kuonyesha taharuki.

Mazrui (1981) pia ametumia sajili ya sheria katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Anasimuliwa kuhusu kesi ya msichana wa kishamba aliyetafunwatafunwa na majibwa ya bwana shamba kwa sababu alipitia kwa shamba lake. Bwana shamba hakushtakiwa. Sajili ya sheria imetumika katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* kuonyesha vile sheria hutumiwa kulinda maslahi ya wachache dhidi ya waliowengi. Sheria iliyopo ni ya

ukandamizaji. Aidha, msamiati wa kisheria umetumiwa mara nyingi kama vile sheria (uk 3), kesi (uk.3) mashtaka (uk 21), wakili (uk 76), Lanina wa Muyaka, mashtaka yako... yanahusu mauaji. (uk 74-75), na kadhalika. Ni kupitia kwa matumizi ya sajili hii ambapo mwandishi ameendeleza maudhui yake ya kuonyesha vile sheria inatumiwa kulinda maslahi ya wenye mamlaka (Delamon) huku ikiwakandamiza watawaliwa (Lanina na wengine)

Bakhtin (1973, 1981 na 1986) anasema kwamba kila tamshi ni jibu la kitu kingine na hutarajiwa kujibiwa. Kwa hivyo kila tamshi huwa ni usemezano kwa sababu ni jibu lililotolewa baadaye au kabla. Kwa sababu watu huzungumzia mambo ambayo tayari yamezungumziwa (Bakhtin, 1986). Mazrui (1981) ametumia sajili ya mazungumzo katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Tamthilia ya *Kilio Cha Haki* inaanza kwa mazungumzo kati ya Dewe na Musa. Wanaendelea kujadiliana huku Dewe akiendelea kumsomea Musa gazeti naye Musa akiendelea kujibu. Kwa hakika, hisia za uchungu zinajitokeza wanaposoma habari kwamba Lanina amewekwa kizuizini kwa madai ya kuongoza mgomo ulioleta mauaji ya akina Delamon. Mara nyingi wanakatizana usemi hasa Musa anapofoka kwa hamaki mpaka Dewe anashindwa kama ataendela kumsomea au la (uk 1-5). Mazungumzo pia yanadhihirika kati ya Delamon na askari wake Kimbo na Shari ambapo kuna kuchanganya ndimi (uk 9 -10, na 12), kuna mazungumzo kati ya Lanina na Mwengo (uk 29 – 35), wazazi wa Lanina na Lanina na kadhalika. Ni kupitia kwa mazungumzo ya wahusika tofauti ambapo tunafahamu hisia zao na misimamo yao. Katika mazungumzo haya inadhihirika kuwa Dewe na Musa wanajibizana, Delamon na askari wake wanajibizana, Lanina na Mwengo wanajibizana, wazazi wa Lanina na Lanina wanajibizana na kadhalika. Uwili wa muelekeo unajitokeza kati ya wahusika hawa kutokana na mazungumzo yao. Katika mazungumzo ya Dewe na Musa muelekeo wa Dewe ni kuwa ili mapinduzi yafanikiwe kunahitaji uvumilivu na umaakini sio kuwa na hamaki na kufanya mambo haraka haraka kama vile Musa alivyokuwa akitaka kufanya. Mazungumzo haya ni kama wanayajibu matukio ya umma kwamba ingawa mgomo umetokea na akina Lanina wamekamatwa wataendelea na mapigano kwa hivyo huo sio mwisho. Kama vile hakuna kauli ya mwisho basi kumuweka Lanina kizuizini sio mwisho. Tunaweza kuchukua kana kwamba mazungumzo haya ni jibu kwa Delamon kuwa hajafanya lolote kwa kumshika Lanina kwani sasa ndio mapambano yatawaka moto zaidi.

Tukiendelea kauli ya Bakhtin (1986) kwamba hakuna kauli ya mwisho tunaona kwamba mazungumzo kati ya Lanina na wazazi wake ni ya kisemezo. Babake Lanina anamuasi kwa sababu ya kukiuka mila na utamaduni (uk 37-42) naye Lanina anasema utamaduni unaweza kukosolewa kama uko makosani. Hii ni kuonyesha hakuna kauli ya mwisho, sio lazima mtu afungwe na kanuni za utamaduni kwani kila kitu huweza kubadilika. Utamaduni wapaswa kuwa umejifungua na kuwa wazi kurekebishwa kwa maoni ya Lanina. Mazungumzo haya pia yanadhihirisha kauli ya usemezano kuwa ili mazungumzo yawepo lazima kuwepo na msememeza na msemmezwa. Mukarovsky (1977) anasema kwamba mahusiano ya msememeza na msemmezwa huwa na washiriki angaa wawili ambao hutambuana kama “mimi” na “yeye”. Jambo hili linajitokeza katika mazungumzo kati ya wahusika kama vile Dewe na Musa, Lanina na Babake Delamon na Askari wake na kadhalika. Ni katika mfuatano huu wa majibu na majibizano ambapo tamthilia ya *Kilio Cha Haki* inaendelea mbele.

Pierce (1994) akifafanua usemezano ni nini ametoa jazanda ya simu ambapo kuna wahusika angaa wawili, msemaji na msemmezwa. Anasema ya kwamba msemmezwa wa mazungumzo ya simu lazima aonyeshe kuwepo na kusikiliza kwake. Mahitaji ya mawasiliano humlalizimisha kutoa sauti. Kwa hivyo simu inakuwa ni kama ambayo msemaji na msemmezwa huweza kuwasiliana ambapo mmoja huwa ni wa msemaji na upande mwingine ni wa msikilizaji. Kama vile simu, neno ni nafasi iliyoko na inayomilikiwa na msemaji na msemmezwa kwa pamoja na ina sifa ya baina ya....hadhira na mbunaji. Kwa hivyo Mazrui (1981) ametumia sajili ya mazungumzo katika uwasilishaji wa maudhui yake.

Katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* mwandishi ametumia mashairi katika kuwasilisha ujumbe wake. Ushairi unaweza kuwa na sifa mbalimbali kutegemea mtazamo tunaochukulia. Kwa mujibu wa wanamapokea kama vile Abedi (1954) shairi huwa na sifa kama vile sanaa ya vilna na urari wa mizani, ufusaha wa maneno, maneno ya mkato, lugha nzito inayovutia, uvutaji wa moyo, maneno ya hekima, fikira za ndani na lazima liweze kuimbika. Kwa hivyo shairi lolote lile hufuata sheria maalum kama vile vina na mizani, utosheleshaji na kadhalika.

Nao wanausasa (wanamapinduzi) kama vile Kezilahabi (1977), Mazrui (1988) na Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema sio lazima shairi liwe na sifa hizi zote. Wao wanasisitiza zaidi sifa ya lugha na maudhui. Maoni yetu ni kwamba sajili ya shairi huweza kubainishwa kwa sifa kama vile matumizi ya lugha yenye mpangilio na ya mkato, matumizi ya taswira, lugha iwe na mdundo na maudhui mazito yashughulikiwe.

Mtunzi wa *Kilio Cha Haki* ametumia ushairi kueleza hisia nzito na kuendelea maudhui mazito hasa ya ukombozi. Mfano ni kama vile katika (uk 7) ambapo wafanyakazi wanaimba wimbo wa kishairi wakati wamegoma. Ingawa ni shairi huru au wimbo wa kishairi usiozingatia vina au mizani lakini pia kuna mapigo maalum. Kwa kifupi tunaieleza kuhusu udhalimu wa makaburu na vile wafanyakazi wameamua kupigania haki yao kwa matumizi ya lugha ya mkato na yenye taswira. Kwa kifupi tunaweza kusema kwamba mwandishi wa *Kilio Cha Haki* ametumia nyimbo na mashairi katika kuendelea maudhui yake. Takribani wahusika wake wote

amewapa lugha ya kishairi kama vile Lanina, Wafanyakazi, Mzee Ingeli, Delamon na kadhalika. Baadhi ya sifa zilizojitokeza katika mashairi na nyimbo hizi ni vifungu kwa mfano Kwa ujumla Mazrui (1981) ametumia sajili mbalimbali katika utunzi wake. Kuna matumizi ya sajili ya magazeti, sajili ya mazungumzo, sajili ya sheria, sajili ya nyimbo na mashairi na kadhalika. Kwa hivyo sifa ya kuwepo kwa sajili mbalimbali katika riwaya pia ipo katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981) na hivyo basi sifa ya usemezano kama vile katika riwaya ipo katika tamthilia hii.

1.2 ATHARI ZA MATINI MBALIMBALI

Katika usemezano matini mbalimbali huathiriwa na kuhusiana. (Bakhtini 1981). Matini hizi huhusiana kwa kutajwa waziwazi au kuzitumia katika kujifafanua zaidi. Kwa hivyo katika kutaja dhana au kuzieleza ili zifahamike vyema zinaweza kuhusishwa na matini za dini, historia, fasihi na kadhalika. Bakhtin (1986) anasema kauli ni mwagwi wa kauli nyingine na ni katika kufahamu kauli ya pili ambayo lazima ijulikane ile ya mwanzo ilikuwa inasema nini. Mtamkaji hujirekebisha kutokana na kauli ya kwanza na kwa hivyo huathiri matamshi yajayo. Ni katika mukthadha huu wa kuathiriana ambapo tumechunguza jinsi tamthilia ya *Kilio Cha Haki* imeathiriwa na kuathiri matini zingine.

Tukianza na athari za mawazo ya Kirusi, ni dhahiri kwamba wahusika wengi katika *Kilio Cha Haki* wamepewa majina ya Kirusi ambayo yameswahilishwa. Mifano ya majina ya wahusika hawa ni Lanina kutokana na Lenin, Pelekha kutokana na Pelekhanov, Matovu kutokana na Martov, Engeli kutokana na Engels na kadhalika. Tukichukulia mfano wa mhusika mkuu Lanina jina lake linafanana na la Lenin ambaye alikuwa mwanamume na alikuwa shujaa wa mapinduzi yaliyoangusha utawala wa kimwinyi na kibepari, (King'ei, 2001). Watawala hawa waliokuwa wakiitwa Tsars nchini Urusi walikuwa wakatili na walimiliki njia zote za kuzalisha mali kama viwanda na biashara huku wakiwadhulumu na kuwanyonya raia. Lenin aliongoza mapinduzi hayo mnamo mwaka wa (1917) kwa kufuata sera na siasa za kijamaa. Tunaweza kusema kwamba kama Lenin wa Urusi (Lane 1981) alivyoikomboa jamii yake kupitia mapinduzi ya kijamaa, Lanina anajitolea kuongoza wafanyakazi wenzake kujikomboa kutokana na ukatili na dhuluma ya mabepari kama Delamon (King'ei 2001:68).

Mazrui (1981) anafafanua kwamba Lanina ni mshairi aliyemakinika anampa jina Lanina wa Muyaka (uk 2). Tukizingatia kwamba mengi ya maudhui ya Mashairi ya Muyaka yaliwahimiza Wamvita kupigana dhidi ya Pate, Lamu na Unguja walipovamiwa yaani yanahusu ushujaa na kupigana dhidi ya dhuluma ni dhahiri kwamba Mazrui ameathirika na Muyaka ili kuwahimiza wanajamii wake wapigane dhidi ya dhuluma za Delamon na wengine kupitia kwa mhusika Lanina. Ni kupitia kwa ushairi ambapo Lanina anajitokeza kama anayefahamu jamii yake kuwa shida zake zinatokana na udhalimu wa makaburu na vilevile hisia za Mazrui (1981) kwamba aliunga mkono mapinduzi dhidi ya utawala dhalimu na utetezi wa haki za wafanyakazi zinajitokeza.

Tukizingatia kwamba matini huweza kuathiriana mbele na nyuma, (Bakhtin, 1990) tunaweza kusema Mazrui (1981) ameathiriwa na Husseni (1969) na 1971). Katika tamthilia ya *Mashetani* kuna dhana ya ushetani inayoashiria ukoloni au uovu. Mfano ni kama (uk 38) ambapo babake Lanina anamwita bintiye, binti ya shetani kumaanisha binti aliyejaa mawazo ya kizungu ambapo mwanamke na mwanamume huchukuliwa kuwa sawa na kushiriki kwa mambo kama vile siasa na kadhalika. Katika uk 42 tumeona babake Lanina akimwambia anyamaze na asimwambie mawaidha ya shetani hivyo tamthilia ya *Kilio Cha Haki* kama vile *Mashetani* ina matumizi ya dhanaya shetani kuonyesha uovu. Aidha maudhui ya *Mashetanini* mikinzano ya kitabaka, ukoloni, ukoloni mamboleo na ukombozi ambayo pia tumeona kwamba ni baadhi ya maudhui katika *Kilio Cha Haki*.

Aidha tunapochunguza tamthilia ya Kinjeketile (1969) inahimiza Watanzania kupigana dhidi ya dhuluma za Wajerumani. Chini ya uongozi wa shujaa Kinjeketile Watanzania waliungana kupigania haki zao. Vilevile tamthilia ya *Kilio Cha Haki* inazungumzia mapinduzi ambapo tabaka lililomiliki nyezo za ushahishi mali litang'olewa mamlakani na kuunda taifa lenye usawa. Tamthilia zote zinazungumzia vita dhidi ya dhuluma.

Isitoshe inadhihirika kuwa Mazrui (1981) ameathiriwa na matini za kidini katika utunzi wake. Kwa mfano kuna mhusika Musa ambaye pamoja na Dewe walikuwa wamehama makwao baada ya kuongoza mgomo wa Wafanyakazi (uk 1-9). Kwa mujibu wa King'ei (2001) mhusika huyu anaweza kufananishwa na Musa wa Bibilia na Korani katika vitabu vya Dini. Nabii Musa ambaye alitumwa na Mungu kwenda kupambana na Mfalme katili (kama vile Delamon) wa nchi ya Misri aliyeitwa Firauni ili kuwakomboa wana wa Israeli. Kwa mujibu wa Bibilia na Korani wana hao wa Mungu walikuwa wamewekwa na Firauni kama watumwa wake ambao aliwafanyiza kazi za sulubu na kuwatesa kwa kila njia. Musa anajiunga na viongozi wengine ili kupigania haki ya wafanyakazi wengine.

Matini nyingine ambayo inahusiana na *Kilio Cha Haki* ni tamthilia ya Wa Thiong'o na Mugo (1978) Mzalendo Kimathi. Katika tamthilia ya Mzalendo Kimathi, Kimathi anawafukuza wasaliti (uk 44) kama ambavyo Lanina anavyofanya katika *Kilio Cha Haki*. Tukichukulia kwamba tamthilia ya *Kilio Cha Haki* pia inazungumzia usaliti wa vita vya ukombozi basi kuna mfanano na tamthilia ya Mzalendo Kimathi. Isitoshe

baadhi ya mapendekezo ya Lanina na Kimathi ni kujenga taifa lenye usawa ambalo ni wazo la kijamaa. Kwa maoni yao uhuru wa kweli hauwezi kupatikana ikiwa wananchi hawawezi kuzimiliki njia za kuzalisha mali.

Matini nyingine ambayo imeathiriwa na *Kilio Cha Haki* ni *Chembe Cha Moyo* (1988). Wafula (1988) anasema sehemu nyingi za kishairi za tamthilia ya *Kilio Cha Haki* zimedondolewa na mtunzi na kukusanywa kama tungo za ushairi zinazopatikana katika diwani ya *Chembe Cha Moyo* (uk 109). Mfano ni kama wimbo kuhusu chungu (uk 56) ambao umedondolewa neno kwa neno kutoka diwani ya *Chembe Cha Moyo* (uk 18). Kwa hivyo kuna mshabaha mkubwa baina ya tungo zinazopatikana katika mashairi ya *Chembe Cha Moyo* (1988) na *Kilio Cha Haki*.

Tamthilia ya *Kilio Cha Haki* pia inafanana na tamthilia ya Mulokozi (1979) ya *Mukwava wa Uhehe* ambapo mhusika Mtage aliongoza jeshi dhidi ya Wajerumani. Mtage kama vile Lanina ni jemedari wa kike aliyeheshimiwa kwa ujasiri wake. Aidha kuna matumizi ya lugha ya kishairi katika tamthilia zote mbili. Mulokozi anatumia ushairi ili kuzingatia umuhimu wa Mwakilingomutwa kama kitambulisho cha roho ya uhehe. Mazrui (1981) vilevile ametumia lugha ya kishairi kuonyesha umuhimu wa Lanina katika kuongoza mapinduzi kwani wamepevuka kimawazo.

Kuna athari kubwa kati ya tamthilia ya *Kilio Cha Haki* ile ya Mohammed (1995) ya *Amezidi* (1995). Mwandishi wa *Amezidi* ameanza kwa kudondoa ushairi ulio kwenye *Kilio Cha Haki* (uk 5). Katika dondoo hili tunaona Mzee akijisaili ni kwa nini bara hili la Afrika liendelee kundidimia ilhali wanaendelea kulifanyia kazi kila siku.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa tamthilia ya *Kilio Cha Haki* imetumia matini zingine kama vile matini za dini, historia na fasihi ili kuweza kujifafanua zaidi. Aidha mazrui ameathiriwa na watunzi wa Kirusi pamoja na watunzi wengine kama vile Said Ahmed Mohamed katika kazi zake ilhali yeye pia amewaathiri watunzi wengine. Kama vile Bahktin (1986) anavyosema kuwa matini huweza kuathiriana kutoka mbele na nyuma ni dhahiri kwamba Mazrui (1981) ameathiriwa na matini zingine na yeye pia ameziathiri.

1.3 MTAGUSANO BAINA YA NAFSI YA “MIMI” NA “YEYE”

Ili matini iweze kudhihirisha usemezano ni muhimu iwe na sifa ya mvutano baina ya nafsi ya “mimi” na “yeye”. Holoquist (1990) anasema kwamba Bahktin alishikilia kwamba ili kuweza kufahamu “mimi” lazima pia uelewe “yeye”. Daima kila kitu huwa ni usemezano tukizingatia kwamba “mimi” huweza kujielewa kupitia kwa “yeye” na “yeye” huweza kujifahamu kupitia kwa “mimi”. Kwa hivyo ni kama kuna uhusiano wa baina ya... kwa sababu ya mvutano ambao huwepo baina ya nafsi mbili mnapopatikana usemezano.

Katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* kuna mvutano baina ya nafsi ya Watawala na Watawaliwa, Wafanyakazi na Waajiri wao, Polisi na raia, wasaliti na viogozo wa mapinduzi, Wanaume na Wanawake na utamaduni wa Kigeni na ule wa Kiafrika.

Nafsi ya Watawala na Watawaliwa, nafsi ya watawala inawakilishwa na serikali pamoja na mfumo wote wa sheria. Watawala wanawalinda mabepu kama vile Delamon kwa kutumia Polisi na sheria vibaya. Watawala wanawadhulumu Watawaliwa kwa kuwanyima haki za kimsingi kama ulinzi dhidi ya dhuluma za makaburu na mfumo wa sheria unatumia kuwanyima haki raia ili wasiweze kujitetea. Mfano ni kama katika (uk 7) ambapo tunaarifiwa kuhusu msichana aliyetafunwa na majibwa wa Bwana shamba na hakuchukuliwa hatua yoyote. Ni katika mivutano ya nafsi hizi mbili ambapo msomaji wa tamthilia ya *Kilio Cha Haki* anaelewa kwa kweli katika jamii anayozungumzia Mazrui (1981) kuna ukosefu wa haki na kuna kilio kweli ili haki iweze kutekelezwa kama vile kukamatwa kwa Bwana shamba na kuhukumiwa. Aidha, kupitia kwa mvutano huu baina ya nafsi ya polisi na raia (wafanyakazi) ambapo tunang’amua kwamba katika jamii ya *Kilio Cha Haki* polisi hawatekelezi kazi yao ipasavyo wao wanatumia tu kulinda maslahi ya matajiri kama vile Delamon. Kwa upande mwingine nafsi ya wapiganaji haki kama vile Lanina inakinzana na ile ya polisi kwani Lanina angetaka kuona haki ikitekeleza.

Kuna mtagusano baina ya nafsi ya waajiriwa na waajiri wao. Hali hii inawakilishwa na Delamon ambaye nia yake ni kupata faida nyingi iwezekanavyo huku akiwanyonya wafanyakazi wake kwa kuwalipa mishahara duni. Kwa upande wao wafanyakazi wanataka kazi lakini wanaona wanadhulumuwa na Bwana Delamon. Ni dhahiri kwamba nafsi hizi mbili zinategemeana na kuhusiana. Wafanyakazi hawataki kufutwa kazi kwani wanategemea mishahara wanaopata kukidhi haja zao lakini kwa upande mwingine wanaona wamalipwa mishahara duni ndipo baadhi yao wanaamua kupigania haki zao sio za mishahara tu bali hata za hali ya kikazi. Kama vile Lanina anavyosema sio mishahara mdogo ambao hudunisha bali ni hali ya kazi yenyewe.

Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba katika jamii ya *Kilio Cha Haki* kuna mivutano baina ya Waajiri (Delamon) na Waajiriwa (Lanina, Dewe na Musa) na ni kupitia kwa mivutano hii ambapo tunaolewa uhusiano wao uko vipi. Ni uhusiano mbaya ambao unadunisha. Vile vile kupitia kwa mivutano baina ya nafsi hizi mbili ndipo mnatokea Wasaliti kama vile Tereki ambao wasaliti Wafanyakazi wengine baada ya kushawisha kufanya hivyo. Naye Delamon anatumia hila kama vile kuunda chama cha kutetea haki za wafanyakazi na kuwaongeza mishahara huku akitoa kwa upande mwingine.

Katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* kuna mivutano baina ya nafsi ya kiume na ya kike. Nafsi ya kiume inawakilishwa na watu kama vile Mwengo, Delamon, Seromanga (babake Lanina) na kadhalika. Kwa upande mwingine nafsi ya kike imewakilishwa kupitia kwa Lanina na mamake. Kwa kweli kuna ukinzani dhidi ya nafsi hizi mbili ambapo nafsi ya kiume imetawaliwa na taasubi ya kiume nayo nafsi ya kike imetawaliwa na mawazo ya kiukombozi. Ni kupitia kwa mivutano baina ya nafsi hizi mbili ambapo uhusiano baina ya jinsia ya kike na ya kiume unaeleweka katika jamii ya *Kilio Cha Haki*. Tukichunguza nafsi ya kiume ni yenye ubinafsi na kujipenda. Mwengo kwa mfano anachukulia kwamba majukumu yote ya nyumbani ni ya Lanina na kwa hivyo Lanina hapaswi kujishughulisha na mambo ya siasa lakini ashughulikie jamii yake. (uk32)

Nafsi ya kiume na ya kike zinapingana na kuhusiana kwani ingawa Mwengo na Lanina wanapingana bado wanaendelea kuhusiana. Ni kupitia kwa uhusiano wa nafsi hizi mbili ambapo tunaelewa kuwa katika jamii ya *Kilio Cha Haki* mwanamke anakandamizwa maradufu kama mfanyakazi na kama mwanamke kwa sababu ya uana wake. Hata hivyo, kwa maoni yetu mwandishi anasemazana na jamii ya kike kwamba ingawaje wangetaka kujikomboa sio lazima wavute sigara kama Lanina au wavunje ndoa zao. Aidha, sio lazima wanaume ambao wanashirikiana na wanawake katika ukombozi wabadilisha mitazamo yao kabisa kama vile Mwengo anavyobalishwa na Lanina. Wanaume wanaweza kushiriki katika ukombozi wa akina mama kwa kujadiliana nao na kuwasikiliza ili masikizano yawepo.

Kupitia kwa mivutano ya nafsi ya Watawala na Watawaliwa, Polisi na raia, Waajiri na Wafanyakazi, Wanawake na Wanaume ambapo Mazrui amedhihirisha uhusiano uliopo baina ya nafsi hizi zote ni wa unyanyasaji. Ni nafsi ambazo zinategemeana na kuhusiana kwa namna fulani katika hali zote. Bara la Afrika au mataifa ya Kiafrika yanahitaji Mataifa ya Kigeni na Mataifa ya Kigeni yanawahitaji kama vile Delamon alivyohitaji wafanyakazi nao wanamhitaji. Kupitia kwa mivutano hii uhusiano baina ya nafsi hizi unajitokeza kama uhusiano ulio baina ya ---. Ni katikati ya ambapo maana huweza kupatikana baina ya uhusiano wa “mimi” na “yeye” na ni kweli kwamba sifa hii ya usemezano ipo katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981).

1.4 MASIMULIZI YA MOJA KWA MOJA YA KIFASIHI

Mazrui (1981) ametumia masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi ili kuwasilisha ujumbe wake. Ametumia methali, mashairi, nyimbo, mafumbo na kadhalika ili kuweza kuendeleza maudhui yake na kuyafafanua. Kama vile Bakhtin (1981) asemavyo kwamba mwandishi hutumia masimulizi haya ya moja kwa moja katika uandishi wa riwaya sehemu hii tutajuliza iwapo mwandishi wa *Kilio Cha Haki* (1981) ametumia masimulizi haya.

Katika *Kilio Cha Haki* (1981) kuna matumizi mengi ya methali ili kuendeleza maudhui anayowasilisha. Katika (uk 25) tunapata methali kwamba “mhitaji ni mtumwa” kuonyesha kwamba wafanyakazi ni wahitaji na kwa hivyo ni wahitaji wasio na hiari (Njogu 2001: 48). Lanina kwa maoni yake ni kwamba Delamon ndiye mhitaji kwani anahitaji kunyonya na kudhulumu. Katika huendeleza maudhui ya ukombozi, Mazrui (1981) ametumia methali “hasira hasara” ambapo Lanina anasema kwamba hasira haiwezi kuwa hasara kama dhamira yake ni ukombozi. Huu ni ukweli kama kila taifa ambalo huhitaji kujikomboa lazima kwanza hasira iwepo ndipo waweze kupigana na utawala ambao ni dhalimu. Hii pia yadhihirisha kauli ya Bahktin (1990) kwamba kauli zote hupaswa kuwa zimejifungua wala sio kujifunga. Huweza kuleta uwili wa muelekeo na kwa hivyo hakuna kauli ya mwisho au maana ya mwisho. Huu ni ukweli tunapozingatia kwamba katika muktadha mmoja hasira huweza kuwa hasara kama pale mtu anaweza kufanya jambo mbaya sana kwa hasira na mwishowe kujuta. Lakini ni kama ni katika mambo ya kiukombozi ama kujitetea hasira lazima iwepo ili mtu aweze kujikomboa au kujikinga na udhalimu pamoja na maonevu ya aina yoyote ile. Katika muktadha wa *Kilio Cha Haki* hasira inakubalika kwani wanaonyanyaswa sana hasa wanawake kama Lanina ambao wanateswa kila mahali yaani kazini, nyumbani kwa muwewe, nyumbani kwa babake na mwishowe watu wengi katika jamii wanamkataa na kumuuta Malaya. Kwa kweli hasira kwake ni muhimu ili aweze kuutetea utu wake katika jamii ambayo inamuonea vilivyo.

Kuna methali nyingi ambazo Mazrui (1981) ametumia kama vile kila kiovu hulaaniwa (Uk 36), dalili ya mvua ni mawingu (uk 36), mkosa chema hawachi kuguna (uk 37),

Midomo ya waja haichoki kusema (uk 36), kizuri hakiwachi kutiwa ila, na kadhalika. Mwandishi ametumia methali hizi kuweza kufafanua maudhui yake zaidi na kuelezea mawazo ya wahusika wake. Katika matumizi ya methali ambazo zinapingana na dhamira ya ukombozi kama vile hasira hasara mwandishi anasemazana na hadhira yake kwamba iwapo fasihi ni nzuri kama vile methali pia huweza kutumiwa kupumbaza watu wasijikomboa. Kwa hivyo kuna umuhimu wa kufikiria zaidi juu ya maandishi ya kifasihi kwa kutafakari na kuyahakiki upwa sio kuyafuata kiholelaholela au kikasuku.

Hii ina maana kuwa ni lazima fasihi ijiweke wazi kunakidiwa na kurekebisha na wanajamii kama vile Bakhtin (1990) anavyosema lazima methali hizi zihakikiwe, zirekebishwe na kutumiwa katika muktadha ufao. Kauli ya Bakhtin (1986) kwamba Adamu tu ndiye aliyeanza neno la kwanza na kwa hivyo maneno mengine huwa ni miangwi ya maneno mengine basi hakuna neno la mwisho. Hata methali sio lazima iwe eti vile

imesema ni hivyo. Inaweza kurekebisha au kukataliwa au kuleta maana nyingine katika muktadha tofauti na hivyo ni usemi ambao umejifungua.

Maandishi mengine ya kifasihi ambayo mwandishi ametumia ni nyimbo na mashairi. Wahusika wengi kama vile Lanina, wafanyakazi, mzee Ingeli, Delamon na kadhalika wanapewa lugha ya kishairi katika mazungumzo yao. Kama King'ei (2001) anavyosema, nyimbo na mashairi hutumiwa sana kwani huwa na athari kubwa sana kihisia kwani husisimua na kuwa nadharia ya kuvuta hadhira yake.

Kwa hakika nyimbo na mashairi yametumika sana hasa pale ambapo wafanyakazi wanafanya mgomo (uk 7, uk 8, uk 9, uk 13) na kadhalika na pale ambapo Lanina au wahusika wengine wanapoendeleza mawazo ya kifalsafa na ya kidini pia wametumia lugha ya kishairi (uk 56, uk 64, uk 62) na kadhalika.

Takribani wahusika wote walio katika *Kilio Cha Haki* wamepewa lugha ya kishairi. Isitoshe kila mara wafanyakazi wanapogoma wanaimba nyimbo zenye maudhui ya ukombozi. Aidha Lanina anapowahutubia mara nyingi ametumia lugha ya ushairi ili kuwavutia na kuteka hisia zao. Kwa kweli Mazrui (1981) ametumia nyimbo na mashairi moja kwa moja katika kuendeleza maudhui yake.

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba Mazrui (1981) ametumia maandishi ya kifasihi moja kwa moja katika kazi yake kama vile methali, mafumbo, nyimbo na mashairi kwa kiasi kikubwa hivi kwamba mtu asomapo tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981) anahisi mdundo katika tamthilia nzima. Huenda ikawa ni kwa sababu Mazrui (1981) pia ni Mshairi na kama vile tulivyosema maudhui mengi yaliyoshughulikiwa katika diwani ya mashairi ya *Chembe Cha Moyo* (1988) yanafanana sana na maudhui yanayoshughulikiwa katika *Kilio Cha Haki*. Ni kupitia kwa matumizi ya masimulizi haya ambapo mwandishi anasisitiza jukuma la fasihi katika kuzindua jamii na vile vile kuonya kwamba masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi kutoka kwa mwandishi katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* na kwa hivyo usemezano upo.

HITIMISHO

Katika makala hili tulilenga kubaini ikiwa usemezano upo kwenye riwaya kinyume na kauli ya Bakhtin (1981) kuwa usemezano hupatikana kwenye riwaya pekee. Kwa kutumia tamthilia ya *Kilio Cha Haki* tumeweza kuonyesha kuwa usemezano huwepo katika tamthilia. Sifa za kisemezano zilizojitokeza ni kwamba tamthilia ya *Kilio Cha Haki* ni mkusanyiko wa sajili mbalimbali kama vile sajili ya magazeti, sajili ya mazungumzo, sajili ya nyimbo na mashairi. Aidha, imebainika kuwa atika *Kilio cha Hakikuna* athari za matini zingine ambazo zinatajwa na kutumiwa katika kujifafanua. Matini kama vile za kidini, kihistoria na kifasihi zinahusiana na zimeathiriwa na matini ya *Kilio Cha Haki*. Jambo lingine ambalo linajitokeza ni kwamba, Mazrui (1981) ametumia masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi katika uwasilishaji wa ujumbe wake kama vile methali,

Nyimbo, mashairi na kadhalika. Ametumia masimulizi haya kwa ufundi mkubwa hivi kwamba yanaingiliana vizuri na kujalizana. Sifa nyingine ambayo imejitokeza katika tamthilia hii ni mtagusano baina ya nafsi ya "mimi" na "yeye". Kuna mivutano baina ya nafsi ya Watawala na Waajiri wao, Wanaume na Wanawake na kadhalika. Imebainika kwamba kupitia kwa mivutano hii ambapo maana hupatikana kwani hatuwezi kuzungumzia mwanamke bila kuzungumzia mwanamme, hatuwezi kuzungumzia bara la Afrika bila kuzungumzia Mataifa ya Kigeni na kadhalika na kwa hivyo maana huweza tu kudhihirika panapo ukinzani baina ya "mimi" na "yeye". Ni kauli yetu kwamba, kama sifa hizi zimo katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* usemezano upo kama vile katika riwaya. Sifa hizi zinaingiliana, kutegemeana na kujalizana ili kuunda tamthilia nzima.

MAREJELEO

- [1]. Abedi, K.A. (1954) Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri Nairobi: East African Literature Bureau.
- [2]. Bakhtin, M.M. (1981 Ed) *The Dialogic Imagination: Michael Holoquist*.
- [3]. (Mhariri) Austin: University of Texas Press
- [4]. (1984 Ed) *Problems of Dostoevsky's Poetics. Theory and History of Literature Vol. Minneapolis: University of Minnesota Press.*
- [5]. (1986 Ed.) *Speech Genres and other late Essays. Austin University of Texas Press*
- [6]. (1990) *Art and Answerability. Austin: University of Texas Press.*
- [7]. Clark, K & Michael, H. (1984) *Mikhail Bakhtin, Cambridge: Harvard University Press.*
- [8]. Haji, I.A. (1981) "Wahakiki wameachwa nyuma na kazi za Fasihi" Makala
- [9]. Aliyotoa katika Semina ya fasihi na Isimu iliyotayarishwa na Taasisi ya Kiswahili ya Lugha za Kigeni" Zanzibar.
- [10]. Hirschkop, K and David, S (1989) *Bakhtin and Cultural Theory. Manchester: Manchester University Press*
- [11]. Holoquist, M (1990) *Dialogism: Bakhtin and His World. London: Routledge. Hussein I (1971) Mashetani. Dar-es-Salaam: Oxford University press Kamunde M.E (1983): "Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Saidi Ahmed Mohammed" M A Thesis (unpublished) University of Nairobi.*

- [12]. Karama, R.M. (1996). "Al-Inkshafi: Ushahidi wa Usemezo Katika Ushairi wa Kiswahili" M A Thesis (unpublished) Kenyatta University.
- [13]. Kezilahabi, E (1976) Ushairi wa Shaaban Robert. Nairobi: Kenya Literature Bureau
- [14]. King'ei G.K. (1997) Mwongozo wa Amezidi. Nairobi: East African Educational Publishers.
- [15]. Lane, D(1981) Leninism: A Sociological Interpretation Cambridge: Cambridge University Press
- [16]. Lofchie, (1965) Zanzibar: Background to the Revolution: New Jersey Princeton University Press
- [17]. Lukacs, G (1963) The Meaning of Contemporary Realism. London Merlin Press
- [18]. Mazrui, A (1981) Kilio Cha Haki Nairobi: Longman
- [19]. (1988) Chembe Cha Moyo. Nairobi: Longman
- [20]. Medvedev P.N & Bakhtin M.M (1978) The Formal Method in Literacy
- [21]. Scholarship: A Critical Introduction to Sociological Poetics
- [22]. Baltimore: John Hopkins Press
- [23]. Mlamba, P. (1983) Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania
- [24]. Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
- [25]. Mulokozi, M (1979) Mukwawa Wa Uhehe. Nairobi: East African Publishing House
- [26]. Mulokozi, M na Kahigi, K (1979) Kunga za Ushairi na Diwana Yetu. Dar es Salaam
- [27]. Tanzania Publishing House
- [28]. Mukarovsky, J (1977) The World and the Verbal Art: Selected Essays. New
- [29]. Haven: Yale University Press.
- [30]. Mohammed, S.A (1974) Vito vya Hekima: Maneno ya Mshangao. Nairobi: Longman
- [31]. (1978) Asali Chungu. Nairobi: Shungwaya.
- [32]. (1980 a) Dunia Mti Mkavu. Nairobi: Longman.
- [33]. (1980b) Utengano Nairobi : Longman
- [34]. Morson, C. 1980 (Mhariri) Bakhtin Essays and Dialogues of His Work:-
- [35]. Chicago: The University of Chicago Press
- [36]. Morson, G.S Caryl. (1990) Mikhail Bakhtin, Creation of Prosaics Stanford University press
- [37]. Mosoti, Z.M. (1993) "Maudhui Katika Tamthilia nne za Emmanuel Mbogo
- [38]. M.A Thesis (Unpublished) University of Nairobi
- [39]. Mugambi, P.J.M (1982) "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili
- [40]. Za Kikunya Zilizochapishwa" Tasnifu ya M.A
- [41]. (Haijachapishwa) Nairobi, Chuo Kikuu Cha Nairobi
- [42]. Muindi, A(1990) "Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Riwaya za Said
- [43]. Ahmed Mohammed" Tasnifu ya M.A (Haijachaoushwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- [44]. Mukobwa, M. (1985) "Maendeleo ya Kimaudhui Katika tamthilia tano za
- [45]. Ebrahim N. Hussein" Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Nairobi, University of Nairobi
- [46]. Mule K. (1991) "Swala la Mwanamke Katika Tamthilia za Kiswahili:
- [47]. Waandishi wa Kike katika Njia Panda". Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Chuo kikuu cha Kenyatta
- [48]. Ndung'u, V(2001) "Uchanganuzi wa Usemi katika Sajili ya Dini: Sifa Bainifu za
- [49]. Lugha ya mahubiri" Tasnifu ya MA (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta Nairobi.
- [50]. Njogu, K. (1986) Mwongozo wa Mukwawa wa uhehe. Nairobi: Heinemann
- [51]. Njogu, k. (1993) "Dialogic Poetry: A Contestation and Social Challenge
- [52]. In East Africa Poetic Genres" PhD Thesis (Unpublished)
- [53]. Yale University.
- [54]. (1997) Mwongozo wa Amezidi Nairobi: Longman Kenya
- [55]. (1997) Uhakiki na riwaya za visiwani Zanzibar
- [56]. Nairobi: University Press Njogu, K na chimerah, R (1999) Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi
- [57]. Jomo Kenyatta Foundation Njogu, K (2001). Mwongozo wa Kilio Cha Haki. Nairobi: East African Educational
- [58]. Publishers
- [59]. Pearce, L. (1994) Reading Dialogics. Toutledge: Chapman and Hall inc
- [60]. Rodney, W. (1972) How Europe Underdeveloped Africa. Dar-es-salaam: Tanzania
- [61]. Publishing House
- [62]. Topan, F. (1971) Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Kitabu cha
- [63]. Kwanza: Nairobi Oxford University Press
- [64]. (1977) Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili Kitabu cha Pili Oxford: Oxford University Press.
- [65]. Wa Thiong'o, N na M. Mugo (1978) Mzalendo Kimathi Nairobi Heinemann
- [66]. Wafula R.M (1999) Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo Yake Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.